



Australian Government



# Ujauzito, kunyonyesha, na chanjo za COVID-19

Chanjo za Comirnaty (Pfizer) na Spikevax (Moderna) zinashauriliwa kwa wanawake wajawazito na wanaonyonyesha na wanaopanga kupata mimba. Wanawake wanaweza kupokea chanjo katika hatua yoyote ya ujauzito.

Hatari ya matokeo makubwa na mabaya kutokana na COVID-19 (UVIKO-19) ni kubwa zaidi kwa wanawake wajawazito na mimba yao. Wanawake wajawazito wanaopata COVID-19 wana hatari zaidi ya kuhitaji kwenda hospitali au kuhitaji huduma kwa wagonjwa mahututi. Mimba yao atakuwa na uwezekano kubwa zaidi kidogo ya kuzaliwa kabla wakati wake (kuzaliwa kabla ya ujauzito wa wiki 37) na kuhitaji kwenda hospitali kwa kutunzwa.

Kuchanjwa ni njia bora ya kupunguza hatari hizi. Utahitaji dozi mbili za chanjo ya Pfizer, wiki tata hadi sita mbali, au dozi mbili za chanjo ya Moderna, wiki nne hadi sita mbali.

Utafiti kutoka Marekani, wa zaidi kuliko wanawake wajawazito 35,000 ulionyesha madhara baada ya kuchanjwa yalifanana sana kwa wote wanawake wajawazito na wasio wajawazito. Kuchanja hakuongezeki uwezekano wa matatizo kama vile kujifungua mapema, kuzaliwa kwa mtoto aliyekufa, mdogo kwa umri wake wa ujauzito na kasoro za kuzaliwa.

Kadiri data ya COVID-19 juu ya wanawake wajawazito inavyoongezeka, tutaendelea kusasisha ushauri wetu.

## Je! Madhara yanayowezekana ni nini baada ya kupata chanjo ya COVID-19 ya wakati wa ujauzito?

Madhara ya kawaida yanayofuata chanjo za COVID-19 ni pamoja na:

- homa
- mkono wenye maumivu
- kichwa kuumwa
- maumivu ya misuli
- maumivu ya viungo
- baridi.

Ikiwa una madhara yoyote hayo baada ya chanjo yako, unaweza kutumia paracetamol ili kupunguza madhara hayo ya kawaida. Paracetamol ni salama katika hatua zote za ujauzito.

Utafiti kutoka kote ulimwenguni haujagundua madhara yoyote ambayo ni maalum kwa wanawake wajawazito au watoto wao. Hata hivyo, inawezekana kwamba kuna madhara ya adimu sana ambayo watafiti hawajagundua bado.

## Je! Kuna faida yoyote kwa mtoto wangu kutokana na kupata chanjo ya COVID-19 wakati wa ujauzito?

Wanawake wajawazito wenye COVID-19 wana hatari kubwa ya kuzaa mtoto aliyekufa au kujifungua mapema (kabla wakati). Watoto wao wana uwezekano zaidi kuonyesha dhiki wakati wa kuzaliwa, au kuhitaji matibabu katika eneo la watoto wachanga wagonjwa mahututi la hospitalini.

Kuchanjwa ni njia bora ya kupunguza hatari hizi.

Ushahidi wa kisayansi unadokeza kwamba kingamwili inayotengenezwa na wanawake wajawazito baada ya kupokea chanjo ya COVID-19 inaweza kuvuka placenta, hasa kwa wanawake waliopokea dozi zote mbili kabla mtoto wao alizaliwa. Kingamwili hizi zinaweza kumpa mtoto mchanga na kinga kadhaa dhidi ya COVID-19 kwa miezi michache ya kwanza ya maisha.

## Je! Mapendekezo kwa wanawake wanaonyonyesha ni nini?

Pfizer na Moderna zinapendekezwa kwa wanawake wanaonyonyesha. Unaweza kuendelea kunyonyesha kabla au baada chanjo yako.

## Je! Mapendekezo kwa wanawake wanaopanga mimba ni nini?

Pfizer na Moderna zinapendekezwa pia kwa wanawake wanaopanga ujauzito. Kupata chanjo kabla ya kushika mimba kunamaanisha una uwezekano wa kupata kinga dhidi ya COVID-19 wakati wa ujauzito. Tafadhali kumbuka kuwa:

- Huna haja kuepuka kuwa mjamzito kabla au baada ya kupata chanjo ya COVID-19.
- Kuchanjwa hakuathiriki uzazi.
- Huna haja kupata kipimo cha ujauzito kabla kupata chanjo.

## Kwa habari zaidi

Ili kujua mahali ambapo unweza kupata chanjo yako ya COVID-19, tembelea <https://covid-vaccine.healthdirect.gov.au/>

Ikiwa una maswali kuhusu chanjo za COVID-19, zungumza na daktari wako, enda kwa [health.gov.au/covid19-vaccines-languages](https://health.gov.au/covid19-vaccines-languages), au piga simu kwa Simu ya Msaada wa Virusi vya Korona ya Kitaifa kwa 1800 020 080.



Kwa huduma za ukalimani, piga simu kwa 131 450.